# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA

# MAMLAKA YA UDHIBITI WA UNUNUZI WA UMMA

PPRA
Public Procurement Regulatory Authority

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na: GA.128/192/01/"G"/21** **19 Septemba, 2023**

Wazabuni wa Bidhaa na Huduma Mtambuka

**YAH: TAARIFA KWA WAZABUNI WA BIDHAA NA HUDUMA MTAMBUKA**

**Somo: KUJISAJILI KWENYE MFUMO WA USIMAMIZI WA UNUNUZI WA UMMA (NeST)**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

2. Mamlaka inapenda kuwafahamisha Wazabuni wa Bidhaa na Huduma Mtambuka nchini kuwa mfumo wa (Tanzania e-Procurement System of Tanzania – TANePs) utafungwa mnamo tarehe 30 Septemba, 2023 na Utaratibu wa kushiriki kwenye zabuni za vifaa na huduma mtambuka kupitia Wakala wa Ununuzi wa Umma (GPSA) umejengwa ndani ya mfumo (NeST) na utasimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA).

3. Ushiriki wa Wazabuni kwenye zabuni zitakazotangazwa na Taasisi za Umma yaani bidhaa na huduma mtambuka, wazabuni wanapaswa kujisajili kwenye mfumo mpya wa Usimamizi wa Ununuzi wa Umma wa NeST kupitia anuani ya https://www.nest.go.tz. Baada ya kukamilisha usajili na kuidhinishwa "approved" kwenye biashara wanazofanya "business lines", wazabuni hao watapaswa kuingia kwenye sehemu ya "framework agreement" na kusaini vigezo na masharti (Terms and Conditions) ya kutoa huduma ya vifaa na huduma mtambuka kwa Taasisi za Serikali kupitia biashara walizoidhinishwa.

4. Mamlaka inawasisitiza Wazabuni wanaotoa huduma ya vifaa na huduma mtambuka kujisajili kwenye mfumo wa Usimamizi wa Ununuzi wa Umma NeST kabla ya tarehe 30 Septemba, 2023 ili kuweza kushiriki kikamilifu kwenye zabuni za vifaa na huduma mtambuka (common used items and services). Baada ya tarehe tajwa hakutakuwa na mbadala wa kushiriki kwenye zabuni hizo isipokuwa kupitia NeST.

5. Kwa maelekezo zaidi tafadhali wasiliana na dawati wa huduma kwa wateja kwa namba +255736494948 au barua pepe support@nest.go.tz.

Eliakim C. Maswi
**AFISA MTENDAJI MKUU**

Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma

Jengo la Kambarage, Ghorofa ya 9, Barabara ya PSPF, S. L. P 2865, 41104 Dodoma TANZANIA
Simu: +255 26 2963854, Barua Pepe: ceo@ppra.go.tz, Tovuti: www.ppra.go.tz